

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vitaanza Jumatatu tarehe 14 na kuendelea hadi tarehe 27 Januari 2019, Jijini Dodoma. Aidha, Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Bajeti zitaanza vikao vyake tarehe 7 Januari, 2019.

Shughuli zote za Kamati katika kipindi hicho zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Uchambuzi wa Miswada mitano (5) ya Sheria iliyopelekwa kwenye Kamati tatu za Kudumu za Bunge pamoja kupokea Maoni ya Wadau kuhusu Miswada ya Sheria.
- (ii) Uchambuzi wa Taarifa Mbalimbali za Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika Mashirika na Taasisi mbalimbali nchini.
- (iii) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu za Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- (iv) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa za Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- (v) Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.
- (vi) Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

- (vii) Maandalizi ya Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019.
- (viii) Kamati tatu za Ardhi, Maliasili na Utalii, Kamati ya Kilimo, Kamati ya Mifugo na Maji na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa zitakutana pamoja siku ya Ijumaa tarehe 25, Januari, 2019 kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa ya kisékta kuhusu Hali ya Migogoro ya Ardhi nchini.

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge zinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz.

Imetolewa na: Kitengo cha Habari, Elimu kwa Umma na Mawasiliano,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.
03 Januari, 2019.